TANGAZO LA SERIKALI NA. 652 la tarehe 8/9/2023

SHERIA YA KODI YA MAPATO,
(SURA YA 332)

# AMRI

*(Imetelowa chini ya kifungu cha 10)*

AMRI YA MSAMAHA WA KODI YA ZUIO KWENYE HUDUMA YA USHAURI ELEKEZI KWENYE UHANDISI KATIKA MRADI WA UANZISHAJI WA KIWANDA CHA KUZALISHA GYPSUM PLASTER NA GYPSUM PLASTER BOARD NA UPANUZI WAKE KWA KAMPUNI YA KNAUF GYPSUM TANZANIA YA MWAKA 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Kodi ya Zuio kwenye Huduma ya Ushauri Elekezi kwenye Uhandisi katika Mradi wa Uanzishaji wa Kiwanda cha Kuzalisha Gypsum Plaster na Gypsum Plaster Board na Upanuzi wake kwa Kampuni ya Knauf Gypsum Tanzania ya Mwaka 2023.

Msamaha

2. Kodi ya zuio kutokana na huduma za ushauri elekezi kwenye kwa mradi wa uanzishaji wa kiwanda cha kuzalisha gypsum plaster na gypsum plaster board na upanuzi wake inayopaswa kulipwa na Kampuni ya Knauf Gypsum Tanzania inasemehewa.

Ukomo

3. Amri hii itafika ukomo tarehe 26 Juni, 2024 na inaweza kuongezewa muda kwa mujibu wa masharti ya mkataba wa utekelezaji baina ya Kampuni ya Knauf Gypsum Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwakilishwa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania wa tarehe 29 Machi, 2023.

Dodoma,
25 August, 2023

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU
*Waziri wa Fedha*